

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS**

Anwani ya Simu: **"TUME"**
DAR ES SALAAM
Namba ya Simu:0738166703
Fax: 255 - 022 – 246011
Baruapepe:
secretary@psc.go.tz
Tovuti: www.psc.go.tz



TUME YA UTUMISHI WA UMMA,
6 MTA A WA ALBERT LUTHULI,
KITALU NAMBA 10,
S.L.P. 9143,
DAR ES SALAAM.

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

**RUFAA 75 ZILIZOWASILISHWA TUME NA WATUMISHI WA
UMMA ZIMETOLEWA UAMUZI**

Tume ya Utumishi wa Umma imetoa uamuzi wa Rufaa **75** na lalamiko **1** zilizowasilishwa na watumishi mbalimbali wa umma ambao hawakuridhika na uamuzi uliotolewa na Mamlaka zao za Ajira na Mamlaka za Nidhamu.

Tume ilihitimisha rufaa hizo katika Mkutano wake Namba **1** kwa mwaka wa fedha 2020/2021 uliofanyika hivi karibuni Jijini Dar es Salaam. Kati ya rufaa **75** zilizotolewa uamuzi na Tume rufaa **42** zilikataliwa; rufaa **9** zilikubaliwa; rufaa **4** zilikubaliwa kwa masharti kwamba zikashughulikiwe upya na Mamlaka zao za Nidhamu kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu. Aidha, rufaa **20** zilikataliwa kwa kuwa ziliwasilishwa nje ya muda uliowekwa kwa mujibu wa Sheria.


Kwa upande wa malalamiko, Tume ilipokea na kutoa uamuzi wa lalamiko **1** ambapo lalamiko hilo lilikataliwa.

Katika mkutano huu, ilibainika kuwa miongoni mwa makosa yaliyosababisha Watumishi wa Umma kuchukuliwa hatua na Mamlaka zao za Nidhamu ni pamoja na kushindwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo; kukiuka maadili ya utumishi wa umma; kufanya vitendo vinavyodhalilisha utumishi wa umma; uzembe; uoro kazini bila ruhusa ya mwajiri; kujipatia ajira kwa njia ya udanganyifu na kutoa taarifa za uongo kwa mwajiri kwa kufanya udanganyifu katika

ujazaji wa fomu za Mapitio na Tathmini ya Wazi ya Utendaji Kazi (OPRAS) kuwa wana elimu ya Kidato cha Nne na kushindwa kuwasilisha vyeti husika kwa ajili ya uhakiki.

Tume ya Utumishi wa Umma inazikumbusha Mamlaka za Ajira na Mamlaka za Nidhamu kushughulikia masuala ya kiutumishi na mashauri ya nidhamu ya watumishi wa umma kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo. Tume pia inawakumbusha watumishi wa umma wasioridhika na uamuzi unaotolewa na Mamlaka zao kuwasilisha rufaa Tume kwa kuzingatia muda uliowekwa kisheria wa kuwasilisha rufaa ndani ya siku 45 tangu tarehe ya kupokea uamuzi. Kutokufanya hivyo kunasababisha rufaa hizo zitupiliwe mbali kwa kuwasilishwa nje ya muda.

Imetolewa na:



Richard M. Cheyo
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
TUME YA UTUMISHI WA UMMA
DAR ES SALAAM
08 Oktoba, 2020